**HOTUBA YA MGENI RASMI DKT MOSES KUSILUKA NAIBU KATIBU MKUU WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWENYE MAHAFALI YA THELATHINI NA TANO YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO HOTUBA YA MGENI RASMI DKT MOSES KUSILUKA NAIBU KATIBU MKUU WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWENYE MAHAFALI YA THELATHINI NA TANO YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO- 24/03/2017**

**MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA MOROGORO,**

**MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA YA MOROGORO,**

**MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA YA MVOMERO,**

**MHESHIMIWA MBUNGE WA JIMBO LA MOROGORO MJINI,**

**MHESHIMIWA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA,**

**MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO,**

**MWENYEKITI WA BODI YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO,**

**WAJUMBE WA BODI YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO,**

**MKUU WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO,**

**WANAJUMUIYA WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO;**

**WAHITIMU WOTE WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO;**

**WAGENI WAALIKWA WOTE,**

**MABIBI NA MABWANA.**

**WATAALAMU KUTOKA HALMASHAURI ZA MKOA WA MOROGORO**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika hapa nikiwa na afya njema kwa ajili ya mahafali ya thelathini na tano ya vijana wetu; pia nakushukuru wewe Mwenyekiti na Bodi yako kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika mahafali haya. Nichukue fursa hii kumshukuru Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine kwa kuitikia wito wa kuja kuungana nami katika shughuli hii muhimu.

**Ndugu Mwenyekiti**

Naomba kumshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo kwa kazi nzuri anayofanya ya kuongoza Bodi na kusimamia majukumu ya Chuo. Nawashukuru na ninawapongeza pia wajumbe wa Bodi ya Chuo kwa kutekeleza wajibu wao vyema. Napenda kumpongeza Bwana Justo Lyamuya kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro.

Napenda kumshukuru Bwana Desderius Kimbe kwa kukiongoza Chuo hiki kwa ufanisi kwa kipindi chote alichokaimu nafasi ya Mkuu wa Chuo.

Nawapongeza sana Menejimenti ya Chuo, Walimu na Watumishi wote wa Chuo kwa ushirikiano mkubwa mliompatia Bwana Kimbe na kwa kazi nzuri mnayofanya ya kutekeleza majukumu yenu katika Chuo hiki.

Uwajibikaji wenu ndio umewezesha kuwa pata wahitimu hawa 171 tunaowatunuku vyeti leo.

Bila ya kuwepo uwajibikaji wenu, utekelezaji wa majukumu ya chuo usingefanikiwa, na leo tusingekuwa hapa kwenye mahafali haya. Ni kutokana na umoja wenu, mshikamano, na nia thabiti ya kutekeleza wajibu wenu ndiyo sababu leo tuko hapa tukiwa na furaha kubwa. Vilevile napenda niwashukuru na kuwapongeza wahitimu na Wafanyakazi kwa kutekeleza majukumu yao kwa vitendo na leo hii matunda yake ndiyo yanayotufanya tukusanyike hapa tukisherehekea.

**Ndugu mwenyekiti,**

Wizara ya Ardhi na Taifa kwa ujumla vinatambua mchango mkubwa unaotolewa na Chuo cha Ardhi Morogoro katika upimaji ardhi, uandaaji ramani za msingi (Base maps) na kubwa zaidi ni kuzalisha wataalam wa upimaji ardhi katika ngazi ya cheti na stashahada. Tunafahamu kuwa pamoja na kutekeleza majukumu yenu vizuri mnafanya kazi katika mazingira magumu katika maeneo mengi. Pamoja na hayo juhudi zenu tunaziona. Hotuba ya Mkuu wa Chuo imeeleza bayana maeneo mbalimbali mliyofanya kazi na kutoa huduma za kitaalamu na ushauri kwa jamii.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Sekta ya Ardhi, ni sekta nyeti kwa maendeleo ya Taifa, wananchi na mtu mmoja mmoja. Hakuna maendeleo bila Ardhi kwani Mwalimu Nyerere alituasa "Ili tuendelee, tunahitaji ***Ardhi, Watu, Siasa safi na Uongozi bora''***. Ardhi aliyoiongelea Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere na ambayo inaweza kutuletea maendeleo ni ile iliyopangwa, kupimwa na kumilikiwa kisheria. Serikali ya awamu ya tano inahimiza uchumi wa viwanda. Na ili mwananchi anufaike na uchumi wa viwanda inampasa apime ardhi yake na amilikishwe kisheria. Kwa mantiki hiyo, mtu au taasisi inayomiliki ardhi inayo nafasi nzuri ya kujiletea maendeleo, kwani Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni mtaji na ni dhamana inayomwezesha mtu kukopesheka kwenye vyombo vya fedha.

**Ndugu Mwenyekiti**

Mchakato wa kupanga, kupima na kumilikisha Ardhi kisheria unahitaji rasilimali nyingi hususani watumishi wenye sifa za kufanya kazi hiyo. Rasilimali watu ni changamoto kubwa katika maendeleo ya sekta ya Ardhi nchini. Chuo hiki kutoa wahitimu 41 wa cheti cha awali, 70 wa cheti na 60 wa Stashahada ni kazi nzuri ya kupongezwa na kila mpenda maendeleo.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Wizara ya Ardhi itaendelea kubuni, kusimamia na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa manufaa  ya vizazi vilivyopo na vijavyo kwa nia ya kuboresha maisha ya Watanzania na kupunguza migogoro ya ardhi kulingana na sheria ,kanuni, na taratibu zilizoainishwa katika sheria za Ardhi Na.4 na Na.5. Faida za kupima na kumiliki ardhi ni nyingi sana, baadhi yake ni hizi:

i. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa inajulikana eneo lake, ina usalama, haina migogoro ya mipaka,matumizi wala umiliki.
ii. Ardhi iliyopimwa ni mtaji na dhamana katika vyombo vya fedha na sheria.
iii. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni tiketi ya kupata mikopo benki;
iv. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni chachu ya maendeleo ya elimu, uchumi na miji;
v. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ina mazingira safi na ni rahisi kwa serikali, mashirika na taasisi kuweka miundo mbinu ya maji, umeme na barabara;
vi. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni kitovu cha uwekezaji wa ndani na nje.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Sambamba na faida nilizotaja napenda niseme kuwa zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha  ardhi linahitaji fedha nyingi.  Kuna baadhi ya

watu wanadhani kazi hiyo ni rahisi, hapana, vifaa vinavyotumika ni ghali sana na kazi yenyewe ni ngumu.  Hivyo nichukue fursa hii kuwahamasisha wananchi kuchangia gharama za upimaji ardhi na uandaaji wa hati miliki ili kuongeza kasi ya upimaji na umilikishaji Ardhi nchini.  Natoa wito kwa Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa mipango ya jumla na kina ya uendelezaji Miji, upimaji wa maeneo ya kutosha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.  Kuwepo kwa maeneo yaliyopangwa na kupimwa kutasaidia kukuza uchumi wa miji yetu, kupunguza msongamano, migogoro ya ardhi isiyo ya lazima na kuboresha miji.  Nafahamu ipo mipango mingi ya kina ambayo maeneo yake hayajapimwa, natoa wito wa kukitumia Chuo cha Ardhi Morogoro na Vyuo vingine nchini kupima maeneo hayo ili wananchi wapate hati miliki za maeneo yao.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kwa kuwa Lengo la Serikali na wananchi wote ni kuona kunakuwa na ardhi iliyopangwa, kupimwa, na kuwekewa miundombinu na huduma stahiki na Wananchi wanatumia ardhi yao kwa maendeleo yao; hivyo ili Serikali iweze kufanya kazi hiyo naomba wamiliki wote wa Ardhi kote nchini kulipa kodi za Ardhi kwa wakati muafaka .  Kodi hizi ni chachu kwa maendeleo ya Taifa na huduma za kijamii hususani kodi ya majengo .  Serikali itachukua hatua kali kwa mmiliki yeyote asiyelipa kodi, hii ni pamoja na kubatilisha hatimiliki yake.  Ujumbe wangu kwa wananchi ni “lipa kodi ya Ardhi uwe na uhakika wa dhamana, mtaji na

mikopo”. Upimaji ardhi unatoa taarifa sahihi na kamili kwa Serikali, Benki, Mahakama, Mashirika, Taasisi na watu binafsi. Taarifa hizi ni; sehemu ardhi ilipo, ukubwa wake, umbile lake , matumizi ya ardhi, jina na anwani ya mmiliki, kodi inayopaswa kulipwa na tarehe ambayo kodi inapaswa kulipwa. Michoro ya upimaji ardhi inahitajika kwa maendeleo ya miundo mbinu yote nchini.

Naomba sana wananchi na mashirika mbalimbali watumie wapima Ardhi (Surveyors) waliosajiliwa kisheria kupima ardhi yao kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Naomba wote wanaotoa huduma za umeme, simu, maji, na ujenzi wa miundo mbinu kutumia ramani za upimaji miliki (Cadastral Survey plans) ili kuelewa wapi wanapaswa kupitisha miundo mbinu hiyo na kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Changamoto zilizoainishwa katika hotuba ya Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Risala ya Wanafunzi ni za msingi. Aidha juhudi, mikakati na majukumu yaliyoelezwa na Mkuu wa Chuo, Wizara inayatambua na itaendelea kuboresha mazingira ya chuo hatua kwa hatua kadiri bajeti na uchumi wa nchi unavyokua. Ili kuongeza mapato ya Chuo, napendekeza Wakufunzi na Wanataaluma kutumia fursa ya kutoa ushauri (consultancy) na utafiti (research), kwani hii ndio njia pekee na rahisi ambayo inaweza kuvutia wahisani. Naomba Halmashauri zote nchini ziwatumie wataalamu wa Chuo ili kupunguza migorogoro ya ardhi inayowakabili wananchi.

Aidha kuhusu kujenga madarasa, mabweni na nyumba za wafanyakazi, na uendelezaji wa eneo la ekari 33 Mlimakola kwa lengo la kukipanua Chuo, Wizara itaindelea kufanya kila linalowezekana hatua kwa hatua ili kupatikane fedha za kufanikisha zoezi hilo.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Ni sera ya Taifa kuwaendeleza watumishi wake wa kada mbalimbali hivyo Wakufunzi na wafanyakazi watumie nafasi hiyo kila inapotokea ili kukuza ujuzi wao na kupata mbinu mpya za kupambana na changamoto nyingi. Ili Chuo kiendelee, kinahitaji wafanyakazi wenye uwezo kitaaluma, Njia pekee ya kuwapata ni kuwajengea uwezo hao waliopo.

Natoa wito kwa wadau wa elimu kusaidia ufadhili wa mafunzo kwa Wakufunzi na wafanyakazi. Wizara itaendelea kugharamia mafunzo hayo kadiri inavyoweza sambamba na uanzishwaji wa kozi mbalimbali zenye tija kwa Watanzania. Aidha matatizo ya miundo mbinu ya Chuo kama vile mabweni na madarasa Wizara itaendelea kuyashughulikia mwaka hadi mwaka.

**HITIMISHO**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Mwisho nawashukuru tena uongozi wa Chuo kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Mgeni Rasmi. Nawashukuru wazazi kwa kugharamia ada za mafunzo ya watoto wao, nawashukuru wafanyakazi na wanajumuiya wote wa Chuo cha Ardhi Morogoro kwa kuendelea kuchapa kazi kwa bidii. Nawashukuru majirani na wadau wa ardhi kwa kutumia huduma za ardhi pamoja na kulipa kodi. Kwa wahitimu nitakaowatunuku vyeti nawaasa muwe raia wema na watendaji wanaofuata sheria, epukeni rushwa, ufisadi na mjikinge na ugonjwa hatari wa ukimwi. Zingatieni pia mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa kuendelea kutafuta elimu. Elimu ni uhai, haina mwisho na tunu ambayo ukipata hakuna atakayekupokonya. Ni vyema mkajiandaa na kozi ya Shahada mara itakapoanza. Kwa wanafunzi mnaobaki naomba muongeze bidii ya masomo, dumisheni nidhamu, amani, utulivu na ushirikiano na Wakufunzi. Epukeni migomo kwani inarudisha nyuma maendeleleo ya elimu

**Nawatakieni nyote sherehe njema na Baraka tele katika kuendeleza Chuo chetu na Taifa letu kwa ujumla.**

**Asanteni kwa kunisikiliza na sasa niko tayari kuwatunuku vyeti wahitimu wa leo.**

**MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA MOROGORO,**

**MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA YA MOROGORO,**

**MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA YA MVOMERO,**

**MHESHIMIWA MBUNGE WA JIMBO LA MOROGORO MJINI,**

**MHESHIMIWA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA,**

**MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO,**

**MWENYEKITI WA BODI YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO,**

**WAJUMBE WA BODI YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO,**

**MKUU WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO,**

**WANAJUMUIYA WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO;**

**WAHITIMU WOTE WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO;**

**WAGENI WAALIKWA WOTE,**

**MABIBI NA MABWANA.**

**WATAALAMU KUTOKA HALMASHAURI ZA MKOA WA MOROGORO**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika hapa nikiwa na afya njema kwa ajili ya mahafali ya thelathini na tano ya vijana wetu; pia nakushukuru wewe Mwenyekiti na Bodi yako kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika mahafali haya. Nichukue fursa hii kumshukuru Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine kwa kuitikia wito wa kuja kuungana nami katika shughuli hii muhimu.

**Ndugu Mwenyekiti**

Naomba kumshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo kwa kazi nzuri anayofanya ya kuongoza Bodi na kusimamia majukumu ya Chuo. Nawashukuru na ninawapongeza pia wajumbe wa Bodi ya Chuo kwa kutekeleza wajibu wao vyema. Napenda kumpongeza Bwana Justo Lyamuya kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro.

Napenda kumshukuru Bwana Desderius Kimbe kwa kukiongoza Chuo hiki kwa ufanisi kwa kipindi chote alichokaimu nafasi ya Mkuu wa Chuo.

Nawapongeza sana Menejimenti ya Chuo, Walimu na Watumishi wote wa Chuo kwa ushirikiano mkubwa mliompatia Bwana Kimbe na kwa kazi nzuri mnayofanya ya kutekeleza majukumu yenu katika Chuo hiki.

Uwajibikaji wenu ndio umewezesha kuwa pata wahitimu hawa 171 tunaowatunuku vyeti leo.

Bila ya kuwepo uwajibikaji wenu, utekelezaji wa majukumu ya chuo usingefanikiwa, na leo tusingekuwa hapa kwenye mahafali haya. Ni kutokana na umoja wenu, mshikamano, na nia thabiti ya kutekeleza wajibu wenu ndiyo sababu leo tuko hapa tukiwa na furaha kubwa. Vilevile napenda niwashukuru na kuwapongeza wahitimu na Wafanyakazi kwa kutekeleza majukumu yao kwa vitendo na leo hii matunda yake ndiyo yanayotufanya tukusanyike hapa tukisherehekea.

**Ndugu mwenyekiti,**

Wizara ya Ardhi na Taifa kwa ujumla vinatambua mchango mkubwa unaotolewa na Chuo cha Ardhi Morogoro katika upimaji ardhi, uandaaji ramani za msingi (Base maps) na kubwa zaidi ni kuzalisha wataalam wa upimaji ardhi katika ngazi ya cheti na stashahada. Tunafahamu kuwa pamoja na kutekeleza majukumu yenu vizuri mnafanya kazi katika mazingira magumu katika maeneo mengi. Pamoja na hayo juhudi zenu tunaziona. Hotuba ya Mkuu wa Chuo imeeleza bayana maeneo mbalimbali mliyofanya kazi na kutoa huduma za kitaalamu na ushauri kwa jamii.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Sekta ya Ardhi, ni sekta nyeti kwa maendeleo ya Taifa, wananchi na mtu mmoja mmoja. Hakuna maendeleo bila Ardhi kwani Mwalimu Nyerere alituasa "Ili tuendelee, tunahitaji ***Ardhi, Watu, Siasa safi na Uongozi bora''***. Ardhi aliyoiongelea Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere

na ambayo inaweza kutuletea maendeleo ni ile iliyopangwa, kupimwa na kumilikiwa kisheria.  Serikali ya awamu ya tano inahimiza uchumi wa viwanda.  Na ili mwananchi anufaike na uchumi wa viwanda inampasa apime ardhi yake na amilikishwe kisheria.  Kwa mantiki hiyo, mtu au taasisi inayomiliki ardhi inayo nafasi nzuri ya kujiletea maendeleo, kwani  Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni mtaji na ni dhamana inayomwezesha mtu kukopesheka kwenye vyombo vya fedha.

**Ndugu Mwenyekiti**

Mchakato wa kupanga, kupima na kumilikisha Ardhi kisheria unahitaji rasilimali nyingi hususani watumishi wenye sifa za kufanya kazi hiyo. Rasilimali watu ni changamoto kubwa katika maendeleo ya sekta ya Ardhi nchini.  Chuo hiki kutoa wahitimu 41 wa cheti cha awali, 70 wa cheti na 60 wa Stashahada ni kazi nzuri ya kupongezwa na kila mpenda maendeleo.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Wizara ya Ardhi itaendelea kubuni, kusimamia na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa manufaa  ya vizazi vilivyopo na vijavyo kwa nia ya kuboresha maisha ya Watanzania na kupunguza migogoro ya ardhi kulingana na sheria ,kanuni, na taratibu zilizoainishwa katika sheria za Ardhi Na.4 na Na.5. Faida za kupima na kumiliki ardhi ni nyingi sana, baadhi yake ni hizi:

vii. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa inajulikana eneo lake, ina usalama, haina migogoro ya mipaka,matumizi wala umiliki.

viii. Ardhi iliyopimwa ni mtaji na dhamana katika vyombo vya fedha na sheria.

ix. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni tiketi ya kupata mikopo benki;

x. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni chachu ya maendeleo ya elimu, uchumi na miji;

xi. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ina mazingira safi na ni rahisi kwa serikali, mashirika na taasisi kuweka miundo mbinu ya maji, umeme na barabara;

xii. Ardhi iliyopimwa na kumilikiwa ni kitovu cha uwekezaji wa ndani na nje.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Sambamba na faida nilizotaja napenda niseme kuwa zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi linahitaji fedha nyingi. Kuna baadhi ya watu wanadhani kazi hiyo ni rahisi, hapana, vifaa vinavyotumika ni ghali sana na kazi yenyewe ni ngumu. Hivyo nichukue fursa hii kuwahamasisha wananchi kuchangia gharama za upimaji ardhi na uandaaji wa hati miliki ili kuongeza kasi ya upimaji na umilikishaji Ardhi nchini. Natoa wito kwa Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa mipango ya jumla na kina ya uendelezaji Miji, upimaji wa maeneo ya kutosha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na

kijamii. Kuwepo kwa maeneo yaliyopangwa na kupimwa kutasaidia kukuza uchumi wa miji yetu, kupunguza msongamano, migogoro ya ardhi isiyo ya lazima na kuboresha miji. Nafahamu ipo mipango mingi ya kina ambayo maeneo yake hayajapimwa, natoa wito wa kukitumia Chuo cha Ardhi Morogoro na Vyuo vingine nchini kupima maeneo hayo ili wananchi wapate hati miliki za maeneo yao.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kwa kuwa Lengo la Serikali na wananchi wote ni kuona kunakuwa na ardhi iliyopangwa, kupimwa, na kuwekewa miundombinu na huduma stahiki na Wananchi wanatumia ardhi yao kwa maendeleo yao; hivyo ili Serikali iweze kufanya kazi hiyo naomba wamiliki wote wa Ardhi kote nchini kulipa kodi za Ardhi kwa wakati muafaka . Kodi hizi ni chachu kwa maendeleo ya Taifa na huduma za kijamii hususani kodi ya majengo . Serikali itachukua hatua kali kwa mmiliki yeyote asiyelipa kodi, hii ni pamoja na kubatilisha hatimiliki yake. Ujumbe wangu kwa wananchi ni "lipa kodi ya Ardhi uwe na uhakika wa dhamana, mtaji na mikopo". Upimaji ardhi unatoa taarifa sahihi na kamili kwa Serikali, Benki, Mahakama, Mashirika, Taasisi na watu binafsi. Taarifa hizi ni; sehemu ardhi ilipo, ukubwa wake, umbile lake , matumizi ya ardhi, jina na anwani ya mmiliki, kodi inayopaswa kulipwa na tarehe ambayo kodi inapaswa kulipwa. Michoro ya upimaji ardhi inahitajika kwa maendeleo ya miundo mbinu yote nchini.

Naomba sana wananchi na mashirika mbalimbali watumie wapima Ardhi (Surveyors) waliosajiliwa kisheria kupima ardhi yao kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Naomba wote wanaotoa huduma za umeme, simu, maji, na ujenzi wa miundo mbinu kutumia ramani za upimaji miliki (Cadastral Survey plans) ili kuelewa wapi wanapaswa kupitisha miundo mbinu hiyo na kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Changamoto zilizoainishwa katika hotuba ya Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Risala ya Wanafunzi ni za msingi. Aidha juhudi, mikakati na majukumu yaliyoelezwa na Mkuu wa Chuo, Wizara inayatambua na itaendelea kuboresha mazingira ya chuo hatua kwa hatua kadiri bajeti na uchumi wa nchi unavyokua. Ili kuongeza mapato ya Chuo, napendekeza Wakufunzi na Wanataaluma kutumia fursa ya kutoa ushauri (consultancy) na utafiti (research), kwani hii ndio njia pekee na rahisi ambayo inaweza kuvutia wahisani. Naomba Halmashauri zote nchini ziwatumie wataalamu wa Chuo ili kupunguza migorogoro ya ardhi inayowakabili wananchi.

Aidha kuhusu kujenga madarasa, mabweni na nyumba za wafanyakazi, na uendelezaji wa eneo la ekari 33 Mlimakola kwa lengo la kukipanua Chuo, Wizara itaindelea kufanya kila linalowezekana hatua kwa hatua ili kupatikane fedha za kufanikisha zoezi hilo.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Ni sera ya Taifa kuwaendeleza watumishi wake wa kada mbalimbali hivyo Wakufunzi na wafanyakazi watumie nafasi hiyo kila inapotokea ili kukuza ujuzi wao na kupata mbinu mpya za kupambana na changamoto nyingi. Ili Chuo kiendelee, kinahitaji wafanyakazi wenye uwezo kitaaluma, Njia pekee ya kuwapata ni kuwajengea uwezo hao waliopo.

Natoa wito kwa wadau wa elimu kusaidia ufadhili wa mafunzo kwa Wakufunzi na wafanyakazi. Wizara itaendelea kugharamia mafunzo hayo kadiri inavyoweza sambamba na uanzishwaji wa kozi mbalimbali zenye tija kwa Watanzania. Aidha matatizo ya miundo mbinu ya Chuo kama vile mabweni na madarasa Wizara itaendelea kuyashughulikia mwaka hadi mwaka.

**HITIMISHO**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Mwisho nawashukuru tena uongozi wa Chuo kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Mgeni Rasmi.  Nawashukuru wazazi kwa kugharamia ada za mafunzo ya watoto wao, nawashukuru wafanyakazi na wanajumuiya wote wa Chuo cha Ardhi Morogoro kwa kuendelea kuchapa kazi kwa bidii.  Nawashukuru majirani na wadau wa ardhi kwa kutumia huduma za ardhi pamoja na kulipa kodi.  Kwa wahitimu nitakaowatunuku vyeti nawaasa muwe raia wema na watendaji wanaofuata sheria, epukeni rushwa, ufisadi na mjikinge na ugonjwa hatari wa ukimwi. Zingatieni pia mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa kuendelea kutafuta elimu. Elimu ni uhai, haina mwisho  na tunu ambayo ukipata hakuna atakayekupokonya. Ni vyema mkajiandaa na kozi ya Shahada mara itakapoanza. Kwa wanafunzi mnaobaki naomba muongeze bidii ya masomo, dumisheni nidhamu, amani, utulivu na ushirikiano na Wakufunzi. Epukeni migomo kwani inarudisha nyuma maendeleleo ya elimu

**Nawatakieni nyote sherehe njema na Baraka tele  katika kuendeleza Chuo chetu na Taifa letu kwa ujumla.**

**Asanteni kwa kunisikiliza na sasa niko tayari kuwatunuku vyeti wahitimu wa leo.**